

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
BODI YA NAFKA NA MAZAO MCHANGANYIKO TANZANIA



Simu ya Upepo: *Kilimo*” DODOMA” Simu: +255(0) 26 2321192
Barua pepe: info@cpb.go.tz Tovuti: www.cpb.go.tz
Central Business Park, Eneo la Mbugani,
24 Barabara ya VETA,
S.L.P. 337,
DODOMA.



10 Januari, 2024

TANGAZO LA UPANGISHWAJI WA GHALA JIJINI MWANZA.

Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Tanzania (CPB), ilianzishwa ili kufanya biashara ya Mazao ya Nafaka na Mazao mengine mchanganyiko ili kuwa soko la uhakika kwa wakulima. Miongoni mwa majukumu ya Bodi hii, ni kushirikiana na wadau wengine katika utoaji wa huduma kama vile upangaji wa madaraja, ukodishaji wa maghala, huduma za uchakataji ili kuyaongezea thamani mazao na kuyauza katika masoko ya ndani na nje ya Nchi.

Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) inautangazia umma fursa ya upangishwaji wa Ghala No. 3, lililopo Kitalu No. 2A/2 mtaa wa Bohari Nyamagana, Mwanza. Ghala hilo lina ukubwa wa mita za mraba 1,625 kwa eneo la ndani ya ghala kwenye kiwanja chenye mita za mraba 6,000.

Wenye kutaka kupangisha wawasilishe maombi yao wakiainisha;

1. Majina kamili na anuani ya kudumu.
2. Aina ya Biashara anayotaka kufanya.
3. Ofa yake (*Biding price*).
4. Muda anaotaka kupangisha.
5. Nyaraka halali za usajili wa biashara kama vile leseni ya biashara, cheti cha mlipa kodi (Tax clearance) na nyaraka nyengine muhimu.

Maombi hayo yawe yamefika kwenye ofisi za CPB Makao Makuu kwenye anuani iliyooneshwa hapo juu kabla au ifikapo saa 9 Alasiri ya tarehe 20 Januari 2024.

Kwa mawasiliano Zaidi na fursa ya kukagua eneo husika tafadhali wasiliana nasi kwa barua pepe kupitia info@cpb.go.tz au nambari za simu **+255784 362 943**.

WOTE MNAKARIBISHWA

Imetolewa na
MKURUGENZI MKUU
BODI YA NAFKA NA MAZAO MCHANGANYIKO